



**Uanzishwaji wa Mfumo wa Ukusanyaji na Ufuatiliaji wa Takwimu za Sensa (DSS) katika eneo linalotayarishwa kwa ajili ya majaribio ya chanjo ya malaria wilayani Korogwe, Tanzania**

***Kamugisha ML., Ishengoma DRS, Francis F., Mmbando BP. na Lemnge M M***

**Taasisi ya Taifa ya utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Kituo cha utafiti cha Tanga, SLP 5004 Tanga, Tanzania**

**UTANGULIZI**

Mfumo wa ukusanyaji na ufuatiliaji wa takwimu za sensa (DSS) hutumika kufuatilia na kutoa takwimu halisi zinazohusu hali ya afya na matukio mengine katika jamii inayofuatiwa. Takwimu hizi ni muhimu katika kuandaa mipango, kuratibu utekelezaji na kufanya tathmini ya mafanikio ya miradi ya afya inayoendeshwa katika jamii. DSS ilianzishwa katika vijiji 14 vinavyoshiriki katika mradi wa NIMR-AMANET wilayani Korogwe kuanzia Oktoba 2005 ili kutoa takwimu zinatakazotumika katika kuandaa majaribio ya chanjo ya malaria katika vijiji husika.

**UTARATIBU**

Sensa ya msingi ilifanyika Oktoba 2005 ikifuatiwa na mfumo wa kufuatiliaji takwimu za sensa kwa kutembelea kila kaya mara moja katika kipindi cha miezi minne (4) kuanzia Januari 2006. Taarifa zilizokusanywa katika sensa ya msingi ni pamoja na jina la mkuu wa kaya na wanakaya wote, jinsia, tarehe ya kuzaliwa, kazi ya kila mwanakaya, uhusiano na mkuu wa kaya na kabila. Baada ya hapo, ramani za vijiji vilivyoko kwenye eneo la DSS ziliandaliwa kwa kutumia utaalamu wa kompyuta. Katika ufuatiliaji, takwimu zinazokusanywa zinahusu vifo, mimba, uzazi, uhamiaji ndani na nje ya eneo la DSS, mabadiliko ya hali ya ndoa, hali ya uchumi wa kaya, chanjo kwa watoto walio chini ya miaka 5 na magaojwa yanayosababisha vifo vingi vinavyotokea katika vijiji vya DSS.

**MATOKEO**

Sensa ya awali ilionyesha kuwa kulikuwa na jumla ya wakazi 25,328 katika kaya 5,853. Hadi Desemba 2008, idadi ya kaya zilifikia 7,043 zikiwa na jumla ya wakazi 28,752 katika eneo lote la DSS ; kati ya hao, 50.9 % walikuwa wa jinsia ya kike. Watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 walikuwa ni asilimia 13.9 ya wakazi wote. Kwa watu wote wenye umri wa chini ya miaka 20, wengi wao ni wanaume [(angalia umbo namba (figure) 1)]. Idadi ya vifo vilivyotokea ilikuwa 683 na kati ya hivyo, 95 (13.8%) vilikuwa vya watoto wa chini ya umri wa mwaka mmoja na vifo vyote vya watoto chini ya miaka mitano vilikuwa 145(21.2%). Vifo vingi (66.8%) vilitokea nyumbani. Wahamiaji wengi (9425) walihama nje ya eneo la DSS ikilinganishwa na wale waliohamia toka nje (4791). Taarifa za hali ya uchumi wa kaya zilikusanywa kati ya Januari na Aprili 2006 kutoka kwenye kaya 5645. Kati ya hizo, 20.23% ya kaya zote zilikuwa masikini sana na 19.98% zilikuwa na hali nzuri kiuchumi.

**HITIMISHO**

Hadi sasa kazi ya DSS inaendelea vizuri na imesaidia kutoa ajira kwa vijana toka vijiji vilivyoko kwenye mradi. Pia imetoa taarifa ambazo zimesaidia sana katika mipango ya majaribio ya chanjo za malaria. Jitihada zinaendelea kufanywa na uongozi wa Taasisi ya Taifa ya magonjwa ya Binadamu ili kupata fedha za kutosha kuiwezesha kazi hii muhimu kuendelea na ikiwezekana kupanuliwa katika vijiji vingine vionavyozunguka mji wa Korogwe.

**Shukrani:** Tunatoa shukrani kwa wakazi wote wa eneo la DSS na viongozi wa vijiji kwa kufanikisha kazi hii pamoja na uongozi wa Wilaya ya Korogwe. Tunawashukuru wafuatao kwa kwa msaada wao; R. Malisa, C. Msokame, MD Segeja, HA Msangeni, SH Sembuche, MD Seth, EK Malecela, R Madebe, AS Rutta, J. Akida, Seth Nguhu, Nasoro Omari na Waingizaji, na wakusanyaji wa takwimu. Kazi hii inafadhiliwa na African Malaria Network trust (AMANET). Kwa maelezo zaidi wasiliana na: Mkurugenzi (NIMR Tanga) [mlemnge@tanga.mimcom.net](mailto:mlemnge@tanga.mimcom.net) (027 264 7957).

Figure 1: Population pyramid in study villages by sex and age groups

